

# Biashara ya Hewa ya Ukaa ya Udongo: Wimbi Jingine la Uporaji wa Ardhi Kaskazini mwa Tanzania?


Ripoti ya utafiti wa

**Muungano na Mshikamano wa Kimataifa wa Wamaasai (MISA)**

Machi 2025

Muungano na Mshikamano wa Kimataifa wa Wamaasai (MISA)

# Watoa Wito wa kusitishwa kwa muda wa Miaka 5 mitano kwa Mikataba Yote ya Hewa Ukaa ya udongo Katika Nyanda za Malisho za Wafugaji Kaskazini mwa Tanzania.



# JUMBE MUHIMU

- **Ardhi ni maisha na Uhai.** Ufugaji wa kuhamahama ni kiini cha utamaduni na maisha wa Wamasai. Ufugaji na mifumo mbalimbali ya uzalishaji wa mifugo imekita mizizi katika nyanda za malisho na mara nyingi ndiyo njia bora zaidi ya kusimamia na kurejesha nyanda hizo za malisho[1]. Kwa sababu hizi, Wamasai lazima waendelee kusimamia na kulinda ardhi yao na mfumo wa Pamoja wa kusimamia maeneo yao ya malisho. Tunahitaji sera rafiki nzuri, mipango na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi inayo akisi ufugaji kama uti wa mgongo wa jamii ya Wamasai, hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. (mimea vamizi, ukame wa muda mrefu);
- Kuibuka haraka kwa biashara ya hewa ukaa Kaskazini mwa Tanzania inaleta (kunazalisha) mkanganyiko na sintofahamu katika jamii, taharuki na migogoro. Biashara hii Inatengeneza mazingira ya rushwa kwa sababu ya fedha zinazolipwa awali na inanayojulikana kama (kishika uchumba);
- Hakuna utaratibu uliowekwa kulinda Ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC); kabla ya kuingia kwenye mkataba wa biashara ya hewa ya ukaa,
- Biashara ya hewa ukaa ya udongo - huenda kusababisha usumbufu na vurugu kubwa katika ufugaji wa asili wa Kimasai na mifumo yao ya matumizi na usimamizi wa ardhi;
- Biashara ya hewa ukaa sio suluhisho la mabadiliko ya hali ya tabia nchi. inahalalisha uharibifu wa mazingira na kuhalalisha utoaji zaidi wa hewa chafu ya kaboni (CO2) kwa nchi zilizoendelea kiviwanda na ki biashara;
- Soko huria la hewa ukaa halidhibitiwi ipasavyo kitaifa na kimataifa. Mfumo wa kisheria wa biashara ya hewa ukaa Tanzania ambao utalinda ipasavyo haki za binadamu za raia wa Tanzania na jamii unapaswa kuwepo. Katika ngazi ya kimataifa, mfumo wa soko huria la hewa ukaa unaoegemea haki za binadamu unahitaji kuelezwa kwa kina.
- Biashara zote za hewa ukaa ya udongo katika nyanda za malisho zinapaswa kusitishwa angalau hadi 2030. Serikali ya Tanzania inapaswa kusitisha mikataba na mijadala yote ya hewa ukaa ya udongo kati ya jamii za wafugaji na wadau wa miradi ya hewa ukaa hadi:- a) mchakato kamili na sahihi wa Ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) iweze kuhakikiwa na b) kanuni za kimataifa na kitaifa zenye msingi ya haki za binadamu zinazolinda haki za watu wa asili ziwekwe kisheria na ziwe takwa la sheria.

*1 Tazama Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Jangwa (2024), Ripoti ya Dhamira ya Mtazamo wa Kimataifa wa Ardhi kuhusu Nyanda za Mali na Wafugaji. Inapatikana kwa: https://www.unccd.int/sites/default/files/2024-05/GLO%20rangelands%20full.pdf.*

*2 Hii inawiana na wito uliotolewa Aprili 2024 na Ripota Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za Watu wa Asili wa kusitishwa kwa masoko ya kaboni ili kusaidia kukomesha ukiukaji wa haki zao za kibinadamu. Tazama: Mtaalamu Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za Watu wa Kiasili atoa wito wa kusitishwa kwa masoko ya kaboni (29 Aprili 2024). Tazama: https://www.twn.my/title2/biotk/2024/btk240406.htm.*

# MUHTASARI WA TAFITI

Muungano na Mshikamano wa Kimataifa wa Wamaasai (MISA) ulifanya uchunguzi wa kina juu ya kuibuka kwa miradi ya biashara ya hewa ukaa ya udongo Kaskazini mwa Tanzania na kuainisha uwezekano wa uporaji ardhi na athari hasi kwa wafugaji wa jamii ya kimaasai. Ripoti hii inachambua miradi mikuu miwili ya hewa ukaa ya udongo ambayo ni - **The Longido and Monduli Rangelands Carbon Project (LMRCP)** chini ya Soil for the Future Tanzania Ltd (SftFTZ) wakifadhiliwa na Volkswagen ClimatePartners na **The Resilient Tarangire Ecosystem Project (RTEP)** chini ya The Nature Conservancy (TNC) – ikilenga Wilaya za Longido, Monduli, na Simanjiro.

## MATOKEAO YA UTAFITI

- **Kukosekana kwa Ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC):** ya Jamii husika Mchakato wa FPIC umegubikwa na kasoro lukuki, zikiwemo ushirikishwaji finyu wa jamii, usiowahusisha wanawake na vijana, na kukosekana kwa uwazi kwenye mikataba. Wanajamii hawana uelewa wa kutosha juu ya biashara ya hewa ukaa, masharti ya mikataba, na athari zake.
- **Kuvurugwa kwa Ufugaji na maisha yao ya kuhamahama:** Miradi ya hewa ukaa inaanzisha mfumo wa malisho kwa mzunguko , Mfumo amabao unavuruga mifumo ya malisho ya asili kwa jamii ya wamaasai, kuhatarisha ufugaji wa kuhamahama amabao ndio uti wa mgongo wa utamaduni wa wamaasai na nyanda za malisho endelevu. Mabadiliko haya yanahatarisha usalama wa chakula na mikakati ifaayo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- **Changamoto ya mapungufu ya sheria na mazingira ya rushwa:** Kanuni zinazosimamia biashara ya hewa ukaa Tanzania hazina masharti ya kutosha kulinda haki zetu za msingi kama watu wa asili katika miradi ya hewa ukaa ya udongo. Kukosekana kwa mfumo wa kisheria wenye nguvu na wazi kumeleta upotoshwaji wa taarifa muhimu ndani ya jamii na kutengeneza mazingira ya rushwa, (kwa mfano, malipo ya awali au “ kishika uchumba “), na utata wa kisheria, haswa juu ya kuvunja mikataba na mgawanyo wa faida.
- **Wasiwasi wa Jamii:** jamii ya kimaasai ipo kwenye shinikizo kali la kuingia kwenye mikataba, kutokana na wadau wa miradi wawili wakubwa wa miradi ya hewa ukaa wanaoshindana kuwasilisha miradi yao kuhakikiwa na taasisi za kiamataifa ya ubora. Kwa hili lazima wasainishe vijiji vichache na kuamalizia nyaraka zao za mikataba na kupeleka ushahidi wa ushirikishwaji na ridhaa ya jamii. Wanajamii wanahofia masharti ya muda mrefu, kupoteza ardhi ya malisho ya pamoja, migogoro ya ndani na baina ya jamii, na mmomonyoko wa utamaduni. Matarajio ya mikataba ya hewa ukaa ya miaka 40 imeleta wasiwasi mkubwa wa kuweka vizazi vijavyo chini ya kifungo cha mikataba ya kilaghai.
- **Vitisho vya Kuporwa kwa Ardhi:** miradi ya hewa ukaa ya udongo ina hatari ya kurudisha historia ya mifumo ya unyang’anyi wa ardhi ya Wamasai, huku ardhi ya jamii ikikaliwa na kuthibitiwa na wawekezaji wa kigeni na nyanda za malisho zikibinafsishwa kama suluhisho lisilo halisi la mabadiliko ya tabianchi.

# MAPENDEKEZO MAHUSUSI

## 1. Kusitishwa mara moja kwa Miaka 5 (Mitano):

MISA inadai kusitishwa mara moja kwa miradi ya hewa ukaa ya udongo kwenye nyanda za malisho za wamasai hadi 2030 ili kuruhusu elimu pana kwa jamii na kuwekwa kwa mifumo dhabiti ya kisheria katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Kusitishwa kwa miaka 5 ni muhimu kwa ulinzi wa haki za wamasai na kulinda mfumo wa matumizi ya ardhi ya Wafugaji.

## 2. Kuimarisha Mifumo ya Sheria na Sera:

- Uwepo wa mfumo wa kisheria Tanzania mahususi kwa miradi ya hewa ukaa ya udongo, kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na ardhi ya watu wa kiasili.
- Kimataifa, kuna haja ya kuwa na mifumo ya kisheria inayosimamia soko huria la hewa ukaa.

## 3. Kuhakikisha uimara wa Ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC): ya Jamii husika:

- Ushirikishwaji wa kina kwa jamii katika michakato yote ya maamuzi, na juhudi za dhati za kuhusisha wanawake, vijana na makundi maalum na wanakijiji kwa ujumla.
- Upatikanaji huru wa kisheria na taarifa sahihi zisizo na upendeleo kuhusu biashara ya hewa ukaa na athari zake.

## 4. Kulinda Ufugaji na uhamaji:

- Miradi ya hewa ukaa lazima iheshimu mifumo ya asili ya ufugaji wa Wamasai na jamii kubaki kwenye kuhodhi na kusimamia matumizi ya ardhi yake.
- Miradi haipaswi kuweka masharti zinazoathiri uhamaji na zinazoathiri ustahimilivu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- Ushirikiano wa pamoja wa nyanda za malisho uzingatiwe kama mkakati katika kukabiliana na ukame na sio kuudhoofishwa.

## 5. Uwazi na Haki katika mikataba:

Mikataba lazima iwe ya haki, uadilifu, ipatikane hadharani, iandikwe kwa lugha ya kiswahili na isiwe na upendeleo kwa wadau wa miradi ya hewa ukaa na serikali.

## HITIMISHO

**Biashara ya hewa ukaa ya udongo Kaskazini mwa Tanzania ni njia nyingine inayohatarisha uporaji wa ardhi ya Wamaasai na inayotishia urithi wa kitamaduni, maisha ya wafugaji na usalama wa chakula kwa wafugaji wa kimaasai.**

Bila ulinzi thabiti wa kisheria, michakato ya uwazi na ridhaa ya jamii, miradi hii inaweza kuongeza migogoro iliyopo, kuleta mvutano katika jamii na kudhoofisha haki ya tabia nchi na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, hakuna ushahidi wa kisayansi unaothibitisha kuwa mabadiliko yanayokusudiwa katika nyanda za malisho yatapelekea uhifadhi wa ziada wa hewa ya kaboni na hivyo kufanya miradi ya hewa ya ukaa kuwa isiyo ya thamani kwa wanunuzi. MISA inasisitiza kuchukuliwa kwa hatua za haraka kwa kulinda haki za wamaasai na kudumisha misingi ya haki ya mazingira na haki jamii .



# YALIYOMO

**UTANGULIZI** ........ **1**

Maono ya Wamasaai juu ya Uhifadhi ........ 1

Biashara ya hewa ukaa: Ni nini kinajiri vijijini? ........ 2

Mbinu ya utafiti ........ 6

Muundo wa Ripoti ........ 6

**MATOKEO MUHIMU YA UTAFITI** ........ **7**

Kutokuwepo kwa Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) ........ 12

Athari Zinazotarajiwa kwa Ufugaji na Uhamaji ........ 15

**MAPENDEKEZO** ........ **22**

**VIAMBATANISHO** ........ **25**

Kiambatisho cha 1: Hali ya Ardhi na hewa ukaa katika Vijiji 11 ........ 25

Kiambatisho cha 2: Uchambuzi Muhimu wa Kisheria wa Makubaliano ya hewa ukaa: ........ 27

**MUUNGANO NA MSHIKAMANO WA KIMATAIFA WA MAASAI MSHIKAMANO (MISA)** ........ **31**



“ Wakati wowote mradi unapokuja kijijini mwetu, tunahitaji kuhusishwa. Sisi wanakijiji ndiyo tunaopaswa kuwa kwenye usukani mwa mradi wenyewe, na hivyo tunahitaji kujua mradi ni wa nini na kiini chake. Tunahitaji kujua faida na hasara zake na tunahitaji kuamua hatima ya mradi sisi wenyewe bila ushawishi toka nje.”

# UTANGULIZI

## MAONO YA WAMASAAI JUU YA UHIFADHI

Mnamo Julai 2024, Muungano na Mshikamano wa Kimataifa wa Wamaasai (MISA) ulianzisha dira ya wafugaji juu ya uhifadhi inayoitwa Dira ya Wamaasai juu ya Uhifadhi.[3] yenye lengo la kuangalia mustakabali wa ardhi, ufugaji, na dhana ya kuishi pamoja na wanyama pori. Malengo ya utafiti huo ni kupendekeza na kuhamasisha njia mbadala ya uhifadhi wa kisasa kuliko ule Uhifadhi wa kikoloni na wa kibepari wa nguvu ambao umekuwa ukilazimishwa kwa jamii ya Wamaasai, na kusababisha uporaji wa ardhi yao na kuvuruga mtindo wao wa maisha. Maono ya utafiti huu yalibainisha pia hatari za wazi zilizopo dhidi ya maeneo yafuatayo: umiliki wa pamoja wa ardhi na matumizi yake, ufugaji, kuishi/kuwepo pamoja kwa mifugo na wanyama pori, utamaduni, afya, usalama wa chakula, kutokomeza umaskini, elimu, jinsia na haki ya wanawake, uwindaji, utalii na biashara ya hewa ya kaboni.

Wakati wa ufafanuzi wa dira ya uhifadhi ya Wamaasai, tuligundua kuwa jamii nyingi za Wamasai zinahofia kulipuka haraka kwa biashara ya Biashara ya hewa ukaa (tazama kisanduku hapa chini kwa ufafanuzi) ambayo itapelekea (yatasababisha) aina nyingine ya upokaji wa ardhi, na kusababisha (kuongeza katika) ongezeko lililopo la maeneo ya uhifadhi, mapori ya akiba, mapori tengefu, vitalu vya uwindaji, na maeneo ya hifadhi ya misitu pamoja. Ili kushughulikia hofu hizi, MISA ilitoa mapendekezo mawili muhimu mnamo Julai 2024: miradi ya biashara ya hewa ukaa lazima ihakikishe ushirikishwaji huru na wa dhati (FPIC) kwa Wamaasai, na miradi hiyo isiingilie au kuvuruga ufugaji au mfumo wa matumizi ya ardhi ya pamoja ya Wamaasai.

Ripoti ya utafiti huu wa biashara ya hewa ukaa ya udongo inajaribu kutoa majibu na mapendekezo dhidi ya hofu ya wamaasai kuhusu biashara ya hewa ukaa. Wakati MISA inajumuisha wadau mbalimbaliwa kimataifa wenye maslahi ya kuwatetea Wamaasai wanaokabiliwa na kufukuzwa kutoka ardhi yao wanachama wengi wa MISA ni Wamaasai. Kwa sababu hiyo tumefanya uamuzi wa kutumia kauli mbiu yetu ya “sisi.... Ardhi yetu, haki yetu, utamaduni wetu” katika ripoti hii.

*3 CarbonSolve ni ushirikiano kati ya wawekezaji watatu: Mark Ritchie, mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Soils for the Future LLC, kampuni ya Marekani ya kupata faida, na mwandishi wa mbinu ya VM0032 ya miradi ya kaboni ya udongo; Timoty Tear, mtaalamu wa uhifadhi wa Kiafrika na Mkurugenzi wa Mpango wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Taasisi ya Utafiti wa Bioanuwai (BRI), shirika lisilo la faida la uhifadhi; na David Evers, Mwanzilishi, Mkurugenzi Mtendaji, na Mwanasayansi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Bioanuwai (BRI). Kwa habari zaidi, angalia:*

# BIASHARA YA HEWA UKAA: NI NINI KINAJIRI VIJIJINI?

Mnamo Januari 2025, MISA ilitembelea vijiji 11 (kumi na moja) katika wilaya za Longido na Monduli ambavyo vilikuwa vikilengwa na wadau wa miradi ya hewa ukaa. Tulizungumza na wawakilishi wa jamii kuhusu kuibuka kwa kasi kwa miradi ya hewa ukaa na athari zinazotarajiwa. Malengo ya mikutano hii yalikuwa:

1. kutathmini iwapo wadau wa miradi ya biashara ya hewa ukaa wanaheshimu sharti la Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC);
2. Kutathmini iwapo mikataba ya hewa ukaa pendekezwa yanaingilia au kudhoofisha ufugaji na uhamaji, upatikanaji wa rasilimali, na elimu ya jadi ya mifumo ya matumizi ya ardhi;
3. Kukuza na kuongeza ufahamu wetu wa pamoja kuhusu miradi ya hewa ukaa ya udongo. Miradi ya hewa ukaa kwenye udongo ni mpya ikilinganishwa na miradi ya hewa ukaa kwenye misitu. Miradi ya hewa ukaa kwenye udongo inalenga kunasa hewa ukaa kwenye udongo kwa kuongeza ukuaji wa mimea katika maeneo ya malisho. (Ukuaji huo wa mimea itapelekea kunaswa kwa hewa ya ukaa kwenye udongo) Biashara hii ni moja ya aina ya miradi ya kaboni zinazotajwa kama miradi ya asili, pamoja na miradi ya upandaji miti na uhifadhi wa misitu.

Katika maeneo tuliyotembelea, kuna wadau wa mradi wawili kwa sasa:

- **Mradi wa Hewa ukaa kwenye Sehemu za Malisho wa Longido na Monduli (LMRCP),** mradi wa Verra #4924, unaotekelezwa na Soils for the Future (SftF) kwa ushirikiano na CarbonSolve LL**C**[4], Volkswagen ClimatePartner, Converge Analytics, na Biodiversity Research Institute. Mradi huu unachukua ardhi hekta 970,000, na una muda wa miaka 40 ya utekelezaji na kipindi cha mikopo na malipo kinachoanzia tarehe 1 Januari 2024 hadi 31 Desemba 2063. Mradi huu unalenga vijiji 49 katika wilaya ya Longido na 10 katika wilaya ya Monduli. Unatumia mbinu ya VM0032, ambayo iliendelezwa na Soils for the Future. Volkswagen ni mwekezaji na mwezeshaji muhimu na mwanzilishi wa mradi huu kupitia Joint Venture Volkswagen ClimatePartners[5]. Katika ripoti hii, tunarejelea mradi huu kama mradi wa SftF. Inapaswa kufahamika kwamba Soils for the Future pia inahusika katika miradi mingine mitatu inayofanana nchini Kenya: a) Northern Kenya Grassland Carbon Project (NKGCP), mradi wa Verra #1468. Masuala ya haki za binadamu yanayohusiana na mradi huu (maarufu kama mradi wa Northern Rangelands Trust (NRT)) nchini Kenya yameelezewa kwa kina[6]. Kesi ya mahakama hivi karibuni iliamua kwamba angalau mojawapo ya maeneo ya uhifadhi yaliyohusika yalianzishwa kinyume cha sheria kwenye ardhi ya pamoja[7]. Mradi wa LMRCP unalenga vijiji 49 katika Longido na 10 katika Monduli. b) Kajiado Rangeland Carbon Project (KRCP), ambao unatekelezwa upande mwingine wa mpaka wa Tanzania na Kenya, unasimamiwa na wadau wa mradi hao hao kwa kutumia mbinu ile ile na unalenga hekta milioni 1.5[8]. Katika ripoti hii, tunarejelea mradi huu; c) Mradi wa Entooma Sida Maasai Mara, pia unahusiana na mradi wa SftF kwenye mpaka wa Tanzania.

*4 https://www.carbonsolve.world/about-carbonsolve-1*

*5 Volkswagen ClimatePartner ni ubia ulioanzishwa mnamo 2022 juu ya utaalamu na uvumbuzi wa washirika wawili wenye lengo moja: upunguzaji wa kaboni na uundaji wa miradi ya hali ya juu - Volkswagen na ClimatePartner UK. Tazama: https://volkswagen-climatepartner.com/*

*6 https://assets.survivalinternational.org/documents/2466/Blood_Carbon_Report.pdf*

*7 https://www.survivalinternational.org/news/14121*


*8 https://assets.survivalinternational.org/documents/2466/Blood_Carbon_Report.pdf*

- **Resilient Tarangire Ecosystem Project (RTEP),** mradi wa Verra #4742, unaotekelezwa na The Nature Conservancy kwa ushirikiano na TerraCarbon na Tanzania People and Wildlife (TPW). Mradi huu unachukua ardhi takriban hekta 830,000 (ndani ya eneo kubwa la mradi ambalo linaonekana kuwa na ukubwa wa takriban hekta milioni 3.5), na una kipindi cha miaka 20 cha mikopo ya awali (kuanzia 1 Oktoba 2020 hadi 30 Septemba 2040) na chaguo la kuongezewa kwa kipindi kingine cha miaka 20. Mradi huu unalenga vijiji 49 na Eneo la Usimamizi wa Wanyama Pori (WMA) katika wilaya za Longido, Monduli, na Simanjiro. Unatumia mbinu ya VM0042, ambayo imebuniwa kwa ajili ya ardhi za kilimo na sio ardhi ya mifugo rangelands. Katika ripoti hii, tunarejelea mradi huu kama mradi wa TNC. Mradi huu unalenga kuendeleza kazi ya awali ya Northern Tanzania Rangelands Initiative (NTRI), ambayo ni juhudi ya pamoja kati ya The Nature Conservancy (TNC),[9] Ujamaa Community Resource Team (UCRT), Tanzania People and Wildlife (TPW), Pathfinder, Honey Guide Foundation, Maliasili Initiative, na Istituto Oikos. UCRT, ambalo ni shirika pekee la wenyeji, limewezesha mchakato wa kupata hati 80 za kimila za umiliki wa ardhi (CCROs) kama matokeo ya juhudi za ushirikishwaji katika usimamizi wa ardhi kwa pamoja. TNC inapata ufadhili kutoka kwa Uk Darwin Initiative ili kuendeleza mradi huu wa kaboni, kama sehemu ya mradi mkubwa wa uhifadhi (DAREX004) katika mfumo wa Tarangire. UCRT, kama mshirika katika mradi wa Darwin Initiative DAREX004, pia limekuwa likiwezesha mafunzo kuhusu mikopo ya kaboni kama sehemu ya mradi wa DAREX004, kwa ufadhili kutoka Uingereza. Mradi huu wa kaboni kwenye udongo unalenga vijiji 49.



9 *TNC ni shirika la uhifadhi lenye makao yake makuu nchini Marekani lililoanzishwa mwaka wa 1951. Imeshirikiana na Africa Forest Carbon Catalyst ili kuharakisha ukuaji wa miradi ya kaboni katika bara la Afrika. Imejitolea kupanua jalada lake ili kujumuisha miradi zaidi ya udongo na kaboni ya buluu, zaidi ya kaboni ya msitu. Tazama ramani ya miradi yote hapa : https://www.nature.org/en-us/about-us/where-we-work/africa/forest-carbon-catalyst/*

Ramani iliyopo hapa chini (Ramani ya kwanza (1) inaonyesha mradi wa TNC kwenye rangi ya bluu na mradi wa SftF kwenye rangi nyekundu. Mradi mwingine wa SftF kwa upande wa Kenya una rangi ya njano. Eneo lote la mradi wa SftF liko ndani ya eneo la mradi wa TNC.




*Ramani ya 1: mipaka ya mradi kulingana na hati iliyowasilishwa kwa Verra na wapendekeza mradi wote wote. ©Survival International*

## KISANDUKU – Biashara ya hewa ukaa ni nini?

Baishara ya hewa ukaa ni kipimo kinachowakilisha **tani moja ya hewa ukaa** (CO2) (au kiasi kilicho sawa na gesi chafu nyingine) ambayo, inadaiwa, inaondolewa kwenye angahewa. Namna moja ya kufikiria miradi ya hewa ukaa ni kama kuwa na kipande cha karatasi kama kipimo cha hewa ya ukaa kinachoashiria kuondolewa kwa hiyo (CO2) kwenye angahewa. Kipande hicho cha karatasi hupelekwa sokoni na kuuzwa au kununuliwa. Biashara ya hewa ukaa inaweza kununuliwa na kuuzwa kwa pesa kwenye Soko la Hiari la hewa ukaa (VCM). Soko **la Hiari la hewa ukaa (VCM)** hufanya kazi nje ya soko la kufuata sheria (soko la utii) (ambapo uzalishaji wa hewa ukaa huwekewa mipaka). Soko la utii linadhibitiwa na taratibu za kimataifa za kupunguza hewa ukaa kama vile EU Emissions Trading System (EU ETS). Kampuni zinazoshiriki kwenye soko la hiari la hewa ya ukaa hazihitaji kupunguza utoaji wa gesi chafu; ni hiari yao tu ila hufidia utoaji wa gesi chafu kwa kulipa fidia kwenye soko la hiari la hewa ya ukaa. Wanafanya hivyo tu ili wasikwepe uwajibikaji wao kwa umma au ili waboreshe taswira yao mbele ya umma. Hivi sasa, hakuna soko la hiari la umoja wa biashara ya hewa ukaa. Wadau wa miradi ya hewa ya ukaa wanaweza kuuza hewa ukaa moja kwa moja kwa wanunuzi, au kupitia mawakala au soko la kubadilishana au rejareja, au kuuza kwa mchuuzi ambaye anaweza kuuza tena kwa mnunuzi[10]**.** Kuna **aina kuu tatu za miradi ya hewa ukaa: ikiwemo:** Technolojia inayolenga kukamata na / kuondosha hewa ukaa, kuwekeza kwenye, nishati mbadala au kuwekeza kwenye nishati fanisi (majiko safi ya kupikia), kuwekeza kwenye teknolojia mahiri na uondoaji wa hewa ukaa kwa njia ya asili. Aina hii ya mwisho ndiyo inayofanya kuwa sehemu kubwa ya namna ya kuondoa hewa ya ukaa. Njia hii ya asili ya kuondosha hewa ya ukaa ni kama kupanda miti, Kuhifadhi misitu na kuhifadhi hewa ukaa ardhini/udongoni. Miradi ya hewa ukaa ya udongo ni teknolojia mpya ikilinganishwa na miradi ya hewa ukaa ya misitu; Teknolojia hii ya hewa ya ukaa kwenye udongo inalenga kunasa hewa ukaa kwenye udongo kwa kuongeza kufunika udongo na nyasi katika nyanda za malisho. Bei **ya hewa ukaa** kwenye Soko la Hiari ni ya chini kuliko kwenye soko la utii/sheria na ina badilika badilika sana. Bei Inategemea aina ya mradi, ukubwa wake, eneo, ubora na manufaa ya pamoja kwa jamii za wenyeji. Bei ya sasa (ya moja kwa moja) ya hewa ukaa inaweza kupatikana hapa . Mnamo tarehe 9 Februari 2025, hewa ukaa inayotokana na asili iliuzwa kwa dola 0.47 kwenye masoko ya hiari. Bei ya wastani ya biashara ya hewa ukaa mnamo 2024 ilikuwa dola 4.80, ikipungua kwa 20% ikilinganishwa na 2023 [11]. Miradi ya Biashara ya hewa ukaa inaratibiwa na mdau wa tatu anayethibitisha biashara hii kwa kutoa cheti cha uthibitisho. Mdau huyo mthibitishaji kama vile Verra au Gold Standard ambao wana wajibu wa kuthibitisha upunguzaji wa utoaji wa hewa ukaa, kwa kutumia mbinu tofauti. Njia hii ya VM0032 ni mbinu iliyoidhinishwa ya Verra ya "kuwepo kwa Nyasi Endelevu kwenye maeneo ya malisho kwa njia ya kudhibiti moto na malisho yenyewe" mradi huu wa kuhifadhi hewa ukaa udongoni ulibuniwa na Soils for the Future kwa ushirikiano na The Nature Conservancy (TNC) na Fauna na Flora International. Teknolojia ya VM0042 ni mbinu mbadala iliyoundwa kwa ajili ya kuhifadhi hewa ya ukaa kwenye ardhi inayotumika kwa kilimo. Miradi ya Biashara ya hewa ukaa imekosolewa vikali katika miaka miwili iliyopita. Utafiti uliochapishwa katika gazeti la the Guardian mnamo Januari 2023 ulibaini kuwa zaidi ya 90% ya biashara ya kufidia ongezeko la hewa ya ukaa kutokana na adhari ya ukataji misitu iliyokuwa ikifanywa na Verra haikuakisi uhalisia wa kupungua kwa hewa ya ukaa pamoja na ripoti kuanisha wasiwasi mkubwa wa kukiukwa kwa haki za binadamu katika mmojawapo wa mradi huo wa hewa ya ukaa[12].

---

*10 https://carboncredits.com/what-is-the-voluntary-carbon-market/#what-is-the-size-of-the-voluntary-carbon-market*

*11 https://carboncredits.com/carbon-credits-in-2024-what-to-expect-in-2025-and-beyond-250b-by-2050/*

*12 https://www.theguardian.com/environment/2023/jan/18/revealed-forest-carbon-offsets-biggest-provider-worthless-verra-aoe*



## MBINU YA UTAFITI

Timu ya wawakilishi 20 kutoka MISA ilitembelea vijiji mbalimbali vilivyolengwa na wadau wa miradi ya hewa ukaa katika wilaya za Longido na Monduli, ikiwa ni pamoja na: vijiji ambavyo vimesaini mikataba au barua za makubaliano, vijiji vinavyojadili na wadau wa miradi wawili, vijiji vilivyopata mafunzo na kuamua kutosonga mbele, na vijiji ambavyo vimesaini lakini baadaye kuanzisha mchakato wa kuvunja mkataba. Katika kila kijiji kati ya 11, MISA iliendesha mikutano ya tofauti ya ziada na a) wawakilishi wa serikali ya kijiji, b) wanawake na vijana, c) wazee, wawakilishi wa kamati ya malisho na viongozi wa kimila.

Matokeo makuu ya utafiti wetu wa dawati la utafiti kwa ushirikiano na wanajamii katika vijiji 11 yamewasilishwa hapa chini.

## STRUCTURE OF THE REPORT

Ripoti hii imegawanywa katika sehemu nne: 1) matokeo makuu; 2) kukosekana kwa ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa-FPIC  3) athari zinazotarajiwa kwa ufugaji na uhamaji; na 4) mapendekezo. Jedwali la 1 katika kiambatanisho linatoa muhtasari wa vijiji vilivyotembelewa, hali ya ardhi yao na ushirikiano wao na wadau wa miradi ya hewa ukaa. Kiambatanisho cha 2 kinatoa uchambuzi wa kisheria kuhusu mikataba tuliyoweza kuzipata ya hewa ukaa ya udongo.

# MATOKEO MUHIMU YA UTAFITI

## Je hii ni aina nyingine ya uporaji wa ardhi?

- **Biashara ya hewa ya ukaa zina athari tofauti kabisa kwa wenyeji kuliko zile za kuondoa kaboni kwa njia ya misitu.** Hasara kuu za namna nyingi ya biashara hii ya hewa ya ukaa kwa wafugaji wa kimaasai bado hazijaeleweka wala kutarajiwa na hasa athari hasi kwa ufugaji wenyewe, haki za ardhi na maisha ya uhamaji.
- Biashara ya hewa ya ukaa ya udongo zinalenga hasa vijiji vyenye, pamoja na hati miliki ya ardhi, hati za kimila za kijiji za umiliki wa ardhi (CCROs) na mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi. Sababu hasa za wadau wa hewa ya ukaa ya udongo ya kuzilenga vijiji vyenye hati za kimila za kijiji za umiliki wa ardhi (CCROs) pamoja na mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi ni kuwa vijiji hivi vimeshakuwa na ramani ya ardhi ya ufugaji katika maeneo yao. Hali hii itawarahisishia sana wadau hawa wa hewa ya ukaa ya udongo kazi yao kwani biashara hii itafanyika katika maeneo ya malisho ya mifugo. Vijiji vingi katika wilaya ya longido na Monduli zinazo mpango huu wa matumizi ya ardhi japokuwa sio zote. Uwepo wa hati za kimila za kijiji za umiliki wa ardhi (CCROs) ambayo kimsingi huongeza uhakika wa usalama wa ardhi ya kijiji lakini kiuhalisia zinaweka vijiji hivi kwenye hatari kubwa ya kupoteza udhibiti wa ardhi yao kwani menjimenti ya ardhi hiyo itahamia kwa wadau wa biashara ya hewa ya ukaa ya udongo pindi mikataba itakaposainiwa.
- Wamasai wamekuwa wakikabiliwa **na kuporwa kwa ardhi yao** tangu enzi za kikoloni. Kutangazwa kwa mbuga za wanyama na maeneo maalumu yaliyohifadhiwa yakiwemo; Mapori ya akiba, mapori tengefu, maeneo ya Usimamizi wa Wanyama Pori (WMAs), na Misitu ya akiba yamekuwa yakiwanyima jamii ya Kimasai kutumia sehemu kubwa ya ardhi kwa maisha ya ufugaji. Miongoni mwa maeneo haya ni: Serengeti/Moru, Loliondo magharibi na kusini/ Pololet, Tara-enger/Tarangire, Alaililai le mwasoni/ Mkomazi, Mkungunero, Entim Oolturot, Mikumi, Sikirari/KIA International Airport na Manyara na Mbuga za Kisongo zilizochukuliwa na Jeshi Monduli. **Katika nchi yote ya Wamaasai, wamaasai wana hofu kubwa ya shughuli yeyote nyingine ambayo itahusisha kuporwa kwa ardhi yao.** Mashaka haya yanazidi pale wadau wa Biashara ya hewa ya ukaa wanapokuwa bega kwa began na wale wa sekta ya Uhifadhi wa wanyama na mbuga za wanyama, The Nature Conservancy (TNC) ni shirika la uhifadhi la kimarekani na wakati huo huo Soil for the Future (SftF) ina usharika mkubwa na mashirika ya uhifadhi kama yale ya Biodiversity Research Institute na TNC asili/ ya awali.
- Maeneo yenye mikataba na Wadau wa Biashara ya hewa ya ukaa zina yamkini kubwa ya kuwa **walengwa wa Biashara na Biodiversity (Viumbe hai)** katika hatua za kule mbele kwa dhana ya kuwa watakuwa (wamasai wa maeneo hayo) wachangiaji wakubwa wa mimea kwa ajili ya wanyama pori. Kwa upande mmoja biashara hizi zinaonekana kuleta kipato kwa kijiji lakini kwa upande mwingine utaleta kizuio na vikwazo vya matumizi ya ardhi kwa jamii ya Kimaasai. Pamoja na hayo biashara ya Biodiversity (Viumbe hai) haipaswi kuonekana kama mwendelezo wa biashara ya hewa ya ukaa ya udongo na hasa kwa sababu zinatumia mbinu na vipimo vinavyofanana na vinadai mbinu na vizuio mbali mbali kwa watumiaji wa ardhi ili kurejesha ekolojia.

## Mashindano Kati ya Wadau wa Miradi ya Hewa Ukaa

- Miradi miwili ya hewa ukaa ya udongo zimelenga maeneo yenye mwingiliano (angalia ramani 1), ambapo eneo lote la SftF liko ndani ya eneo la mradi wa TNC. Wilaya tatu zinazolengwa ni Longido, Monduli, na Simanjiro (ambayo ni wilaya pekee iliyolengwa na TNC peke yake). Mradi wa SftF ulisajiliwa katika Kituo cha Ufuatiliaji wa hewa ukaa cha Tanzania tarehe 5 Julai 2023 na kwa Verra tarehe 12 Januari 2024. Kwa upande mwingine, mradi wa TNC ulisajiliwa katika Kituo cha Ufuatiliaji wa **hewa ukaa** cha Tanzania tarehe 24 Julai 2023 (siku 19 baada ya mradi wa SftF) na kwa Verra tarehe 29 Agosti 2023 (mwezi 6 mapema kuliko mpinzani wake). Hali hii inasababisha mashindano makali kati ya wadau wa miradi wawili na vijiji kuwa lengo la miradi yote miwili.
- Vijiji vinashinikizwa sana kusaini kwa sababu wadau wa miradi wawili wana mashindano ya kuwasilisha miradi yao kwa uthibitisho wa viwango vya kimataifa (hapa inamaanishwa ni Verra/VCS), ambayo ni sharti la kuanza kuuza mikopo ya **hewa ukaa** kutoka kwenye miradi hii. Ili kukamilisha maendeleo yao ya mradi, wanahitaji kusaini na vijiji vichache na kuonyesha uthibitisho wa idhini, yote ndani ya muda fulani. Hali hii inasababisha shinikizo na taharuki kwa jamii, kwani masharti yanayoweza kutumika chini ya miradi yanatofautiana kutoka kwa mdau mmoja hadi mwingine. Hii inahamasisha rushwa kupitia malipo ya awali (ada ya kusaini au **kishika uchumba** cha dola 2 za Kimarekani) kutoka kwa SftF na kuweka vijiji chini ya shinikizo kubwa kusaini.
- Kufikia Januari 2025, chini ya vijiji 10 vimesaini mikataba na SftF. TNC imesaini barua za makubaliano na vijiji zaidi ya 10 na WMA (Eneo la Usimamizi wa Wanyama wa Pori, lililoundwa na vijiji nane). Tunatoa uchambuzi wa awali wa hati hizi za kisheria hapo chini.

“sina habari ya biashara ya hewa ya ukaa kuja kijijini kwetu. Kiuhalisia sijui hata unazungumzia nini. Nilishawahi kusikia juu ya kaboni shuleni lakini sifahamu hata kidogo biashara ya hewa ya ukaa inapaswa kufanana na nini.”



## Taharuki na Mkanganyiko Vijijini

- Vijiji vyote vinapendekezwa kulipwa kile wanachokiita pesa za ushirikiano au kishika uchumba **cha dola 2 za Kimarekani kwa hekta moja** na SftF. Hii ilijumuisha malipo ya moja kwa moja ya shilingi milioni 40-130 katika vijiji tulivyotembelea. Katika sehemu nyingi, 50% ya fedha hii ilitumika kwa kuondoa mimea vamizi kwenye maeneo ya malisho, na 50% iliwekewa akiba kwa ajili ya ujenzi wa shule au kituo cha afya au jengo la serikali ya kijiji. Kugawa fedha nje ya mkataba kunachangia vibaya katika mchakato wa Kukosekana kwa Ushirikishwaji Huru, wa Awali na wa dhati (FPIC) kwani inavuruga na kushawishi maamuzi ya watu.
- Kwa mujibu wa sheria za Tanzania, vijiji vinatakiwa kushiriki katika kuandaa mikataba. Serikali za vijiji ndiyo mamlaka inayohusika na kuandaa, kusaini na kusimamia mikataba ya hewa ukaa. Hata hivyo, tuligundua kuwa Serikali za vijiji zimetengwa katika mchakato wa kuandaa mikataba isipokuwa tu kuhusishwa katika kuamua ukubwa wa ardhi ya malisho inayojumuishwa kwenye mkataba.
- Vijiji vingine vimeingia na kusaini barua ya nia na SftF **wakati havina hati ya vijiji halali** (angalia kiambatisho 1). Hii ni kinyume na kanuni za biashara ya hewa ukaa za Tanzania, Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Hewa Ukaa) ya 2022, zilizorekebishwa mwaka 2023, na ni kinyume na mahitaji ya uthibitishaji ya kimataifa kwani kwa kanuni hizi za mimataifa vijiji hivi havina haki za kisheria kusaini mikataba na kuuza hewa ukaa.
- Kijiji kilichotembelewa, ambacho kinataka kufuta makubaliano yake ya hewa ukaa na SftF, kinakutana na hali ngumu na isiyo ya uhakika kwa sababu mifumo ya upatanishi na malalamiko na mifumo ya kumaliza mkataba hayajaeleweka.
- Katika vijiji vingi, **mratibu wa malisho** ameajiriwa na SftF na kupatiwa pikipiki na simu; huyu anafanya kazi kama mfanyakazi wa SftF. Mchakato wa kuajiri mtu huyu haukuwa wazi kwa watu tuliozungumza nao; uhusiano kati ya mratibu wa malisho na kamati ya malisho ya kijiji pia hauko wazi. Mratibu wa malisho anatarajiwa kutembelea maeneo ya malisho kila siku, kufuatilia mwenendo wa mifugo ndani ya malisho na kuripoti kwa kampuni. Kwa upande wa TNC, kundi la waratibu wa malisho litachaguliwa na kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kundi hili litakuwa na jukumu la kutekeleza utaratibu wa malisho ya zamu na mzunguko, pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya malisho ya msimu, na kukusanya mara kwa mara taarifa kuhusu afya ya ardhi ya malisho, ikiwa ni pamoja na data kuhusu upatikanaji wa lishe ya mifugo. Lengo ni pia kuanzisha taasisi mpya ya kijiji inayoshughulikia malisho[13]. Hata hivyo, ni vigumu kuelewa jinsi hatua hizi zitakavyogongana na mifumo ya jadi ya usimamizi wa malisho.

*13 Tazama mradi wa TNC uliowasilishwa kwa Verra, ukurasa wa 12.*

- Wanajamii (hata kutoka vijiji ambavyo vimepata elimu na baadhi yao wameingia katika makubaliano) wana kutokuelewa na kuchanganyikiwa pakubwa na **ukosefu wa taarifa na taarifa zinazokiuka kuhusu masharti na athari za mikataba** ikiwa ni pamoja na muda wa mkataba, usambazaji wa faida (%), malipo yanayotarajiwa, kumaliza mkataba na miongozo ya kutumia fedha ambazo zitapokelewa na serikali ya kijiji. Wanakosa taarifa ya msingi kuhusu bei ya hewa ukaa kwenye soko la kimataifa, kiwango cha msingi cha hewa ukaa kwenye ardhi yao, jinsi sampuli za udongo zinavyokusanywa na kuchambuliwa, wakati na jinsi watakavyopata matokeo ya maudhui ya kaboni kwenye udongo wao, na idadi ya tani za kaboni zinazotarajiwa kukamatwa/ondolewa kila mwaka mara baada ya kuanzishwa kwa mradi. Aidha, hawakuarifiwa ipasavyo kuhusu mabadiliko yote yanayotarajiwa katika mifumo ya malisho na athari zake (kuanzishwa kwa miraba, mzuguko wa zamu, kulishwa kwa mifugo, n.k.).
- Mikataba ya uhamisho wa haki za hewa ukaa ina **muda wa kutarajiwa wa miaka 40**. Mikataba ya SftF ina kipindi cha awali cha mkataba cha miaka 30 kinachoweza kurefushwa kwa miaka 10, wakati barua za nia za TNC zinataja miaka 20 inayoweza kurefushwa kwa miaka 20. Inafahamika na ni wazi kutoka kwa nyaraka zilizowasilishwa kwa Verra kwamba miradi yote ina msingi wa muda wa kutarajiwa wa miaka 40. Wanajamii wengi wanahofia sana kuingia katika mkataba ambao utaweka majukumu na masharti kwa watoto na wajukuu zao. Muda mrefu wa mikataba ya haki za hewa ukaa unaweza kuzifunga vijiji katika hali ambapo hawawezi kubadili na kurekebisha mpango wao wa matumizi ya ardhi, ambao una uhalali wa miaka 10 (angalia chini).

## Kukosekana kwa Mfumo Dhabiti wa Kisheria

- Mnamo Oktoba 2022, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira alichapisha Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Hewa Ukaa), 2022 chini ya Notisi ya Serikali (GN) No 636, inayoyoashiria ushiriki rasmi wa Tanzania katika biashara ya hewa ukaa ya kimataifa. Marekebisho yalifanywa mnamo Oktoba 2023 chini ya Notsi ya serikali (GN) 721. Kanuni hizi zinaunda mfumo wa taasisi za biashara ya hewa ukaa, mahitaji na hatua za usajili wa mradi wa hewa ukaa (kutoka kwa wazo la mradi hadi utekelezaji wa mradi hadi uthibitisho wa kimataifa), ushiriki wa wadau, na utambulisho wa mpango wa kugawana gharama na faida[14]. Aidha, Miongozo ya Biashara ya Hewa Ukaa ya Kitaifa ilichapishwa Oktoba 2022, ambayo hayana nguvu ya kisheria.[15]
- Kanuni hizi hazikuwa zimeundwa awali kwa miradi isiyo ya msitu na hivyo kuwa ni ngumu kubaini hatima kisheria ya miradi ya hewa ukaa ya udongo. Haijulikani, kwa mfano, kama na jinsi asilimia ya kugawana faida iliyoainishwa kwenye miongozo inavyohusiana na hewa ukaa ya udongo. Aidha, Kanuni hizi zinapendelea uhifadhi na faida kuliko haki za ardhi na za binadamu[16].
- Mabadiliko makuu yaliyotolewa na marekebisho ya 2023 ya Kanuni ni kwamba, katika miradi isiyo ya REDD+ (kama vile hewa ukaa ya udongo), usambazaji wa faida unapaswa kujadiliwa moja kwa moja kati ya mtekelezaji wa mradi na Mamlaka Inayosimamia. Hii ina maana kwamba mkataba wa kugawana faida unategemea kabisa uwezo wa vijiji kujadiliana na TNC na SftF. Hii haiwalindi vya kutosha wanajamii wa eneo husika.

---

*14 Hata hivyo, Kanuni ya 9(c) na 16 inaeleza ushirikishwaji wa washikadau lakini kimsingi inalenga vyombo vya serikali, na kuacha jamii kuwa na nafasi ndogo katika kufanya maamuzi.*

*15 https://www.vpo.go.tz/uploads/publications/sw-1715925778-en-1674038035-National%20Carbon%20Trade%20Guidelines-2.pdf*

*16 Kwa mfano, Kanuni ya 19(2) inaamuru kwamba mapato kutoka kwa miradi ya biashara ya kaboni kutanguliza shughuli za uhifadhi wa mazingira, kuhakikisha kwamba faida za kifedha zinaunga mkono mazoea endelevu. Hii itapunguza uwezo wa vijiji kutumia mapato ya fedha kutoka kwa kaboni kwa vipaumbele au maendeleo yao. Kanuni ya 15 na 17 inaagiza kwamba miradi ya kaboni iambatane na vipaumbele vya uhifadhi wa kitaifa na kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIAs).*

## Mikataba yenye dhuluma

- Uchambuzi wa awali wa baadhi ya mikataba ya SftF ambayo tuliweza kupata inaonyesha kuwa vijiji vimeambiwa kusaini mikataba miwili tofauti: moja ni mkataba uhamishaji wa haki za hewa ukaa na nyingine inahusu mgawanyo wa faida. Pia, tuliweza kuchambua barua za nia ambazo TNC imesaini na vijiji. Mawakili wa MISA walichambua vipengele vyote vya mikataba hii kati ya wadau wa miradi na vijiji na kubaini kasoro nyingi (rejea kiambatisho 2).
- Mashaka makubwa kwenye mikataba ya SftF ni pamoja na: a) kukosekana kwe mchakato mzima wa (FPIC) yaani Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa; b) vipengele vya kusitisha mkataba visivyo wazi na ambazo havijaelezwa vizuri na athari zao; c) Mchakato wa utatuzi wa migogoro unaohusisha serikali ya wilaya una kasoro kwa kwani kuna mgongano wa wazi wa maslahi kwa serikali ya wilaya kwani halmashauri ya wilaya inapata sehemu ya faida inayotoka kwenye mauzo ya hewa ukaa inayouzwa na hivyo hawatakuwa tayari kuona kuvunjwa kwa mkataba. d) ushiriki mwanasheria wa halmashauri ya wilaya kama shahidi na mwezeshaji, inapelekea ukosefu wa uhuru katika mchakato mzima; e) Uwepo wa kipengele cha usiri (confidencial clause) kinchozuia uwepo mchakato wa FPIC yaani Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa. f) Uwepo wa vifungo vinavyoweka kuwepo kwa marufuku ya matumizi mengine ya ardhi wakati wa mkataba.
- Masuala muhimu kwenye barua za nia za TNC ni pamoja na: a) makubaliano kubaki kuwa halali hadi mkataba kamili utakapotiwa saini, na hivyo kijiji kufungwa kisheria katika hali ya kutokuwa na haki kisheria kwa kipindi kisichojulikana, ambapo hakiwezi kutafuta fursa nyingine; b) mchakato wa kusitisha makubaliano haujulikani; c) mchakato wa usuluhishi kuwa mikononi mwa serikali ya wilaya na imeweka mkuu wa wilaya kuwa na mamlaka kamili ya kutatua masuala yoyote ya migogoro, hivyo kuzuia mchakato wa kisheria unaostahili kufuatwa.



## KUTOKUWEPO KWA RIDHAA KAMILI ILIYO HIARI, HURU ILIYOHABARISHWA NA KUSHIRIKISHWA (FPIC)

Kadiri ya sheria za kimataifa za haki za binadamu, Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) inapaswa kuwepo kwenye kila hatua ya mikataba na makubaliano, kutoka kwenye utambulisho wa mradi hadi uundaji, utekelezaji na kufungwa kwake. Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) inapaswa kuwepo kabla ya jamii kuingia kwenye mikataba ya hewa ukaa, na wanajamii wote wanapaswa kushirikishwa. Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Hewa Ukaa), 2022 kama ilivyorekebishwa mwaka 2023, pia inasema (Kanuni ya 18) kwamba miradi lazima ipate Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) kutoka kwa jamii za wenyeji.

Tuligundua kuwa masharti ya kuhakikisha Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) hayapo kama inavyoonyeshwa kama ifuatavyo:

- **Ushirikishwaji haba wa umma** katika mchakato wa elimu, uhamasishaji, uandaaji na ufuatiliaji wa mikataba ya hewa ukaa;
- **Wanaopata taarifa kuhusu biashara** ya hewa ukaa na athari za mikataba ni serikali ya kijiji, huku jamii nyingine ikiwa na uelewa mdogo au kutokuwa na uelewa kabisa, hasa wanawake. Serikali ya kijiji kisheria inapaswa kuwa na wanachama 25 (ambapo 7-8 pekee wanatakiwa kuwa wanawake) na ndiyo chombo cha kisheria chenye mamlaka ya kusaini mkataba wa hewa ukaa kwa niaba ya kijiji. Hata hivyo, pendekezo la mkataba lazima kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Tumebaini kuwa elimu imekuwa ikitolewa kwa serikali ya Kijiji, baadhi ya viongozi wa kimila, wazee mashuhuri au watu wenye ushawishi katika kijiji; watu wanaoshiriki mkutano mkuu wa Kijiji ni idadi ndogo kulinganisha na wanakijiji wote;
- **Wanawake na vijana wamejikuta wakiachwa nje** ya mchakato huu na hawashirikishwi wakati wa utoaji elimu ya hewa ukaa na mchakato wa kufanya maamuzi; ushiriki wao katika serikali ya kijiji na mikutano mikuu ya vijiji ni mdogo na haupewi kipaumbele ipasavyo. Kunatakiwa kuwe na mchakato maalum unaoshirikisha wanawake, vijana na watu wengine ambao hawapewi kipaumbele.
- **Hakuna ushirikishwaji wa Wamaasai wengine wote ambao wanaathiriwa na miradi ya hewa ukaa ya udongo** (hata wakiwa nje ya vijiji husika). Hawa wanapaswa kushirikishwa na ushiriki huo uwe huru kwa sababu za athari zinazotarajiwa za mradi hupanuka nje ya mipaka ya kijiji (tazama sehemu hapa chini kuhusu uhamaji na malisho);
- **Kutokuwa na uelewa wa kutosha** juu ya soko la hiari la biashara ya hewa ukaa linavyofanya kazi, muktadha wa kimataifa kukosekana kwa sheria zinazosimamia, na athari za kuingia kwenye mkataba wa biashara ya hewa ukaa. Ukosefu huu wa uelewa umejitokeza katika vijiji vyote isipokuwa kwa baadhi ya wajumbe wa serikali za vijiji ambao wana taarifa zaidi. Ilibainika pia kuwa mashirika ya kiraia na wadau wengine, ikiwa ni pamoja na watunga sera, hawana uelewa wa kutosha juu ya biashara ya hewa ukaa ya udongo;
- **Kukosekana kwa uwazi wa biashara hii ya hewa ya ukaa**, kwani mikataba iliyosainiwa na SftF ina kipengele kinachosema kwamba mikataba hii itakuwa ya siri (kifungu cha usiri); inaonekana kuwa vifungu vya mikataba hii vinawasilishwa kwenye serikali ya kijiji na baadhi ya watu wanaoshiriki mkutano mkuu wa kijiji; hata hivyo, wanajamii hawawezi kuelezea ni vifungu vipi vimejumuishwa kwenye mikataba iliyosainiwa na kijiji chao;

- **Jamii kutokuwa na nafasi ya kupata ushari huru wa kisheria** zaidi ya ushauri kutoka kwa mwanasheria wa halmashauri ya wilaya ambaye ni mfanyakazi wa serikali. Jambo hili linaweza kusababisha mgongano wa maslahi kwa sababu halmashauri ya wilaya pia ni mnufaika wa mgawanyo faida wa mradi wa hewa ukaa;
- **Kutokuwa na taarifa huru na zisizoegemea upande wowote**, kwani wanajamii hupata elimu pekee kutoka kwa wadau wa miradi ya hewa ukaa ambao wana upendeleo wa upande mmoja. Hii inasababisha jamii kutokuwa na nguvu za mazungumzo na maafikiano na kutokuwa katika nafasi ya kushiriki katika kutengeneza mikataba;
- **Kukosekana kwa uhuru kamili** kwa kuwa serikali ya wilaya ni mhusika katika utiaji saini wa makubaliano na mchakato wa usuluhishi. Hii inasababisha mgongano wa maslahi kwa sababu serikali ya wilaya inapata mgawanyo wa faida ya asilimia 8 ya mapato ya biashara ya hewa ukaa;
- **Katika maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori (WMAs)**, barua ya nia inasainiwa kati ya mdau wa hewa ukaa (kwa upande huu TNC) na WMA; mamlaka ya kufanya maamuzi imepokonywa serikali ya kijiji na kupelekwa kwa Mikutano ya Wadhamini (AA) ambayo inahusisha wawakilishi watano kutoka kwa kila kijiji kilichojumuishwa katika WMA. Hakuna mfumo wa kuhakikisha ridhaa ya jamii kwa mradi unaoanzishwa;
- wadau wa miradi ya hewa ukaa hawawasilishi ipasavyo sera zao za Ridhaa kamili iliyo hiari, huru iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) na kutokuepo kwa juhudi zozote za kutekeleza na kuhakikisha FPIC inakuwepo kwa umma.



“Tatizo linaanza pale ambapo hawa wadau wa hewa ya kaboni wanapokuja na wamaasai kama sisi, na hivyo tunawaamini.”

“Mifugo huwa haina na wala haioni mipaka.
Je fedha haitatugombanisha?”



# ATHARI ZINAZOTARAJIWA KWA UFUGAJI NA UHAMAJI.

**Wamasai hawana mipaka.** Uhamaji ni uti wa mgongo kwa ufugaji katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Uhamaji unaongozwa na kuchochewa na upatikanaji wa malisho, maji, na chumvi, na ni utaratibu wa kuhakikisha udhibiti wa magonjwa. Mfumo wa malisho wa asili ya Wamasai hupangwa kulingana na maeneo makuu matatu: nyanda za malisho kwa msimu wa kiangazi, nyanda za malisho kwa msimu wa mvua, na olokeri (maeneo ya ndama, mifugo wagonjwa, na dhaifu). Pamoja na hayo, jamii za Wamasai hushirikiana nyanda za malisho nje ya mipaka ya vijiji kupitia utaratibu wa kimila. Katika miaka ya hivi karibuni, uhamaji wa wafugaji umepunguzwa na upanuzi wa maeneo ya hifadhi, uwindaji, utalii, kilimo, miji na mpango wa umiliki wa ardhi kwa mtu binafsi. Kulindwa kwa ufugaji na uahamaji ni muhimu kwa mustakabali wa ufugaji na maisha yao.

Sheria ya Ardhi ya Kijiji inaweka utaratibu wa kupata na kulinda ardhi ya kijiji kupitia Hati za Ardhi ya Kijiji na Hati za pamoja za haki za kimila za kumiliki ardhi (CCROs). Vijiji vinaweza kupanga matumizi ya ardhi kwa miaka 10, kuamua maeneo ya malisho, maeneo ya makazi na, ikiwezekana, WMAs. Mara tu mpango wa matumizi ya ardhi utakapofanyika, unapaswa kurekebishwa kila baada ya miaka 10. Baada ya kupata CCRO za pamoja na kutangazwa kwenye gazeti la serikali itaweka ulinzi wa ziada kwenye ardhi ya kijiji.
Miradi miwili ya biashara ya hewa ukaa ya udongo ambazo zimejadiliwa katika ripoti hii zimejikita katika nyanda za malisho pekee na sio katika maeneo ya misitu. Miradi ya hewa ukaa inaleta mabadiliko kadhaa kuhusu jinsi maeneo ya malisho yanavyosimamiwa kimila, ili kuleta mabadililiko ambayo kwa kuzalisha hewa ukaa ya ziada utapatikana. Nyongeza ina maana kwamba mradi unatakiwa kuleta manufaa ya hewa ukaa ambayo yasingefanyika ikiwa mradi haukuwepo. Nadharia ya miradi ya hewa ukaa ya udongo nchini Tanzania ni kwamba malisho ya asili yameshusha viwango vya hewa ukaa iliyohifadhiwa kwenye udongo, na kwamba viwango vya hewa ukaa vinaweza kuongezeka na kurejeshwa tena kwa kuanzishwa na kutekeleza aina mpya za malisho yaliyopangwa au ya mzunguko wa malisho wa kasi yaani mzunguko unaobadilika haraka. Pia inasemekana kuwa miradi hiyo italinda maeneo ya malisho yasibadilishwe kwenda kwa matumizi mengine kama vile kilimo, **ingawa hakuna tathmini ya kina ya afya ya udongo** inayopatikana kwa wilaya husika.

Ingawa kuna utofauti mdogo kati ya wadau wa mradi wote wawili wa hewa ukaa ya udongo, lengo lao kubwa ni kuanzisha **malisho ya mzunguko** yenye vitalu vinavyosimamiwa kwa makini na kuendana na msimu. Wanadai kuwa kuachana na mfumo wa kulisha mifugo kwenye eneo mmoja kwa muda mrefu kutasaidia majani ya kutosha kuota katika maeneo ambayo hakukuwa na nyasi.

Ikumbukwe kwamba, dhana hii **inapingana na maandiko ya kisayansi juu ya mada hii**, ambayo inathibitisha kwamba a) hakuna athari kubwa ya malisho ya mzunguko kwenye ongezeko la nyasi, biomasi ya mimea ( yaani ongezeko la mimea kwenye eneo husika ) na uondoshaji wa hewa ukaa hewani na kuhifadhi kwenye udongo na b) kwamba malisho ya mzunguko yanafaa zaidi kwa maeneo yenye mvua za wastani hadi za juu ya wastani, kumaanisha kuwa malisho ya mzunguko haifai kwa maeneo ya hali ya hewa ya ukame na nusu jangwa . Maeneo haya yenye hali ya hewa ya ukame na nusu jangwa ndiyo hasa yanapatikana katika vijiji vya mradi wa hewa ya ukaa ya udongo.[17]

*17 eidi-Jayne Hawkins (2017) Tathmini ya kimataifa ya Malisho ya Pamoja yaliyopangwa TM ikilinganishwa na malisho ya muda mrefu ya msimu: matokeo ya uchambuzi wa meta, African Journal of Range & Forage Science, 34:2, 65-75, DOI: 10.2989/1022017319; Heidi-Jayne Hawkins, Alan Short & Kevin P Kirkman (2017) Je, Holistic Planned GrazingTM hufanya kazi kwenye nyanda za asili?, African Journal of Range & Forage Science, 34:2, 59-63, DOI: 10.2989 /10220119.2017.836732;86732; Richard Teague & Matt Barnes (2017) Usimamizi wa malisho unaozalisha upya utendaji wa mfumo ikolojia na maisha ya malisho, African Journal of Range & Forage Science, 34:2, 77-86, DOI: 10.2989/10220119.2017.1334706*

## Malisho ya mzunguko yanahusu nini?

kanuni kumi muhimu za malisho ya (haraka) ya mzunguko ni:

- kuunda vitalu na kuhamisha mifugo mara kwa mara kutoka kwenye kitalu hadi kitalu (siku 14).
- kuhakikisha mifugo haichungwi kwenye kitalu kimoja zaidi ya mara moja katika kila msimu mmoja wa kiangazi na mara moja katika kila msimu wa mvua.
- kuhakikisha mifugo inaweka nyasi kwa kiwango cha chini ya sm 5-10 (yaani mifugo hazili nyasi zikapungua kipimo hicho) na kuhakikisha hakuna ardhi tupu.
- kuunda makundi mchanganyiko ya wanyama kati ya 50-200 watakoolisha pamoja (wasiwe pungufu au zaidi ili kuhakikisha kuwa nyasi zitakuwepo muda wote na ardhi haitabaki tupu.
- kuajiri na kulipa watu ili kuhakikisha mifugo inahama kwenda umbali mrefu.
- kuhakikisha kwamba ng'ombe, kondoo na mbuzi wote wanahama; hii ina maana hairuhusiwi kufuga kondoo na mbuzi karibu na boma kwa ajili ya maziwa, kwa sababu hii inasababisha uharibifu wa nyasi karibu na maboma.
- Kuhamasisha ufugaji wa kibiashara; kwa upande wa TNC, na kuabadili utamaduni wa ufugaji wa wamaasai kwa kupunguza idadi ya mifugo kutoka kufuga mifugo wengi kwa ajili ya ufahari hadi mifugo wachache ambao utashabihiana na uhifadhi na kutoa fursa kwa wanyama pori kupata malisho kwenye maeneo husika.[18]
- kuwa na mifugo ndani ya eneo la mradi wa hewa ukaa na kuheshimu mipaka ya mradi ili kuepusha uvujaji wa hewa ukaa (kuhamisha mifugo kwenda kwenye maeneo mengine ya malisho yasiyo ya eneo la mradi ambayo yanaweza kusababisha upotevu wa hewa ukaa ya udongo udongoni). Kulingana na mbinu ya Verra VM0032 inayotumiwa na SftF, uvujaji hutokea ikiwa mifugo itasogea zaidi ya kilomita 2 kutoka kwenye mipaka ya eneo la mradi.
- kuajiri waratibu au wasaidizi wa malisho kufuatilia mienendo ya mifugo na kutoa taarifa kila mwezi kwa wadu wa mradi wa hewa ukaa.[19]
- kurekodi na kutoa taarifa ya mabadiliko yoyote kwenye mpango wa malisho, kwa mfano katika suala la moto au ukame.

Wakati baadhi ya vipengele hivi vilitajwa kwa uwazi na wawakilishi wa jamii (kuunda vitalu, kuhamisha mifugo kila baada ya siku 14, kuweka nyasi kwa kiwango cha chini cha sm 10), vingine vinapatikana katika nyaraka za mradi zilizowasilishwa na SftF na TNC kwa Verra au zimefafanuliwa kwa kina katika mbinu (Kanuni) ya Verra VM0032. Ikumbukwe kwamba SftF na TNC hutumia mbinu tofauti (VM0032 kwa SftF na VM0042 kwa TNC) na inaweza kuweka taratibu tofauti kidogo kuhusu masharti ya mipango ya malisho. Hata hivyo, mbinu zote kwa ujumla zinaendana.

*18 DAREX004 AR2 ripoti ya ziada ya mwaka (2023-2024), p.6.*

*19 VM0032, Kupitishwa kwa Nyasi Endelevu Kupitia Marekebisho ya Moto na Malisho. Tazama sehemu ya 8.3.1.1 Uzalishaji wa Uvujajishaji Kutoka kwa Mifugo Waliohamishwa kwenye ukurasa wa 36.*




“Tumesikia kuwa kule ulaya kuna hewa chafu kutokana na viwanda, kwa miradi ya kaboni tunawauzia hewa safi watu wa ulaya ambao kwa ukosefu wa hewa safi hushindwa hata kupumua.”

## Je, jamii ya Kimaasai inahofia nini hasa?

wasiwasi na hofu kubwa zilizoibuliwa na jamii za wafugaji wa Kimasai kuhusu mikataba ya Biashara ya hewa ukaa ni zifuatazo:

- Miradi ya hewa ukaa itazuia kwa kiasi kikubwa **matumizi ya ardhi na uhamaji** na kuvuruga desturi za asili za malisho.
- Miradi ya hewa ukaa itaondoa **desturi ya jadi ya matumizi ya ardhi** na kunyakua ardhi kutoka kwenye udhibiti wa jamii ili kuiweka mikononi mwa mtu wa nje anayetumia sayansi ya Magharibi na kutupilia mbali maarifa ya asili.
- Miradi ya hewa ukaa italeta mbinu zilizoshupaa katika **matumizi ya ardhi na kuzuia jamii kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa njia rahisi.** Wanajamii walieleza kuwa utaratibu wao wa sasa wa malisho na uhamaji unawawezesha na kurahisisha upatikanaji wa maji, chumvi na nyasi. Pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kuendelea na desturi ya uhamaji ni muhimu zaidi kuliko kipindi chochote. walisema. Baadhi pia walieleza kuwa kwa hali ya hewa ya Longido haiwezekani kuweka nyasi katika viwango vya juu ya sentimita 10. (Ni sawa na kupiga marufuka mifugo kula nyasi pekee inayoweza kupatikana).
- Miradi ya hewa ukaa itazuia wafugaji wa **Kimasai kushirikiana na wamaasai wengine kutumia maeneo ya malisho**. Katika mikutano yetu, jamii iliorodhesha maeneo yote ya malisho ya pamoja wanayoyategemea kwa nyakati tofauti za mwaka na kushiriki na Wamasai wengine. Watu wote tuliowahoji waliweza kuainisha maeneo haya kwa kina na pia mipango yao na jamii zingine. Mbali na kutumia kwa pamoja maeneo ya malisho na vijiji jirani, tuligundua kuwa jamii nyingi zinakwenda umbali mrefu kulisha mifugo katika maeneo ya kawaida wanaytumia na Wamasai wengine nje ya vijiji vyao -- hasa wakati wa ukame mkali -- au kukaribisha jamii nyingine kuaa katika maeneo yao. Wana wasiwasi kwamba nyanda hizi za malisho zitajumuishwa katika mojawapo ya miradi miwili ya hewa ukaa ya udongo na hivyo kuwazui kupata malisho kwenye maeneo hayo.
- Miradi ya hewa ukaa **italeta migogoro na mivutano ndani ya jamii na kati ya jamii moja na nyingine.** Mfano ulikuwa kama ifuatavyo. Ikiwa kijiji A kinatumia eneo la malisho na kijiji B alafu kijiji A kinaingia makubaliano ya hewa ukaa, kuruhusu upatikanaji wa mifugo kutoka kijiji B au kuchukua mifugo nje ya mipaka ya mradi kutasababisha hasara ya kifedha. Katika utekelezaji wa ufugaji wa (haraka) wa mzunguko, mienendo ya mifugo itafuatiliwa ili kuhakikisha kuwa a) hakuna uvamizi (mifugo kutoka maeneo mengine inayoingia) na b) hakuna uvujaji (mifugo inayoondoka kwenye mipaka ya mradi). Ingawa hii haitapigwa marufuku kabisa, itasababisha Biashara ya hewa ukaa kuuzwa kidogo, hivyo mapato kidogo ya kifedha. Inaonekana hakuna kipengele chochote katika mkataba wa mradi iliowekwa kushughulikia na kutatua jambo.


- **Miradi ya hewa ukaa itazuia matumizi ya maeneo ya kimbilio hasa nyakati za ukame.** Wanajamii wa Kimaasai walitueleza kwamba huwa wanatenga na kuacha baadhi ya maeneo ya makimbilio ambayo hutumika zaidi katika hali ya ukame mkali. Japokuwa maeneo haya yako ndani ya ardhi ya vijiji (Engaruka, Magadini, Loondolwo, Ngarasero) huwa wanakaribisha na kuwapa nafasi wafugaji kutoka nje ya vijiji hivyo kutumia maeneo haya ya kimkakati. Kwa mfano, tambarare kati ya mlima wa Gilai hadi Oldonyo Lengai nje kidogo ya mlima Kerimasi zinatumiwa na wilaya tatu za Ngorongoro, Longido na Monduli. Wawakilishi hao wa jamii pia walitueleza kuwa waliwapokea wafugaji wa Ndinyika na Sanjan kata ya Malambo, Tarafa ya Sale wilaya ya Ngorongoro kufuatia kufukuzwa kwao kwenye maeneo yao mwaka 2022 wakati tambarare kubwa za Sanjan ulipogeuzwa kuwa Pori la Akiba na wananchi kuachwa bila nyanda za malisho mbadala. Mikutano yetu pia ilibaini kuwa wafugaji kutoka nje ya vijiji hulazimika kujenga boma za muda/msimu (Ronjoi) katika ardhi ya malisho hadi ukame utakapoisha ampapo watarudi vijijini kwao. Watu katika tarafa ya Ketumbeine **(Olopolosek, Orkeju Loongishu, Engushai, Armanie)** wanahofu kwamba iwapo vijiji vinavyozunguka Ngarasero, Oldonyo Lengai na Engaruka wataingia kwenye biashara ya hewa ukaa, itakuwa mwisho wa ufugaji kwao. Ramani za Longido (ramani 2) na Monduli (ramani 3) hapa chini zinaonyesha maeneo ya malisho yanayotumika kwa misimu tofauti[20]. Maeneo ya malisho ni ya pamoja na yanaenea zaidi ya mipaka ya vijiji. Ramani ya 4 inaonyesha njia za mifugo katika wilaya ya Longido. Wakati uhamaji wa masafa marefu ya wafugaji ukishuhudiwa katika wilaya zote, Longido imeongoza zaidi kwa sababu ndiyo wilaya kame zaidi nchini[21].





*Ramani ya 2: Maeneo ya malisho ya Longido yanayotumika katika misimu tofauti ya © DLTP*

*20 Gladness, M., Divine, E., Shirima, GM, Mizeck, C., (2023). Zana ya Usaidizi wa Uamuzi kwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi inayoongozwa na Jamii. https://dtlp.nottech.co.tz/index.html*

*21 Ibid.*




Ramani ya 3: Maeneo ya malisho ya Monduli yanayotumika katika misimu tofauti ya © DLTP




Ramani ya 4: Njia za mifugo Longido © DLTP

**Masuala mengine iliyoibuliwa ni pamoja na:**

- Miradi ya hewa ukaa **hatimaye zitavunja udugu kati ya Wamaasai (Osotwa)** na kusababisha **ubinafsishaji** wa maeneo ya malisho. Wamasai wataacha kutumia malisho kwa pamoja, na kuanza kuambizana kwamba: "Hizi ni nyasi zangu, na hizi ni nyasi zako", kama alivyosema mtu mmoja aliyehojiwa. Wakati athari za mabadiliko haya zikielekea kuwa kubwa, kwa sasa **hakuna mchakato** wa kuhakikisha kuwa kijiji kinachojadili uwezekano wa kuingia mkataba wa hewa ukaa kinahusisha na kushauriana na vijiji vingine vyote ambavyo vitaathiriwa na mikataba ya hewa ukaa kwa vile kwa sasa wanatumia nyanda za malisho kwa pamoja.
- Miradi ya hewa ukaa itaanzisha **mfumo wa pesa za kibepari ambao utaathiri vibaya jamii na utamaduni wa Kimasai** na kupelekea roho ya kutokushirikishana maeneo ya malisho. (Kila mtu afe kivyake).
- Miradi ya hewa ukaa **inaweza kuzuia ujenzi wa boma za muda (Ronjoi)** ndani ya maeneo ya nyanda za malisho au kuzuia matumizi ya miti mitakatifu kiutamaduni.
- Miradi ya hewa ukaa itaanza kuzuia mifugo matumizi ya **nyasi kwenye Nyanda za malisho na wakati huo huo bado wanyamapori hawatazuiwa kutumia Nyanda hizo za malisho.** na kusababisha hasara ya mapato/nyasi; jamii zitapoteza mara mbili: kutakuwa na hewa ukaa kidogo na chakula kidogo kwa ng'ombe, kondoo na mbuzi. Athari kamili za Biashara ya hewa ya ukaa ya udongo hazijaelezwa kwa jamii kikamilifu na hasa uwezekano wa ongezeko la wanyama pori kwenye maeneo yao na mgogoro utakaosababishwa kwa mifugo yao na uwepo wa wanyama hao pori. Hati ya TNC iliyowasilishwa kwa Verra inadai kuwa "Biashara hii ya hewa ya ukaa itasaidia pia kupunguza gharama za uhifadhi wa wanyama pori kwa matumizi ya mbinu hii kwa njia ya mifugo. Itasaidia pia kuongeza upatikanaji wa nyasi kwenye Nyanda za malisho na hivyo kuruhusu wanyama pori wa mbuga ya taifa ya Tarangire kupata nyasi kwenye Nyanda za malisho ya wafugaji wakati wa kipindi chao cha kuhama."29. Hii ina maana kuwa wanyama pori wanategemewa kula mimea kwenye maeneo ya malisho wakati huo huo mifugo haziruhusiwi kupata malisho kwenye maeneo ya WMA's na kwenye mbuga za wanyama pori.
- Jamii itatarajiwa kuandaa mpango wa malisho ambao utapitiwa upya na kuidhinishwa na halmashauri ya Wilaya. Wakati mchakato wa kuandaa mipango ya malisho na kiwango cha ushirikishwaji wa jamii hauko wazi, inahofiwa kuwa mamlaka **iliyonayo serikali ya wilaya ya udhibiti, itatumia fursa ya mchakato huo kimkakati na kuweka marufuku na vizuio kwenye ardhi ya malisho** na hivyo kutenga (kupora) ardhi ya malisho kwa matumizi mengine ya baadaye.



“Tunahofia juu ya migogoro ya ardhi baadaye ambayo yatazaliwa na mradi wa kaboni. Jambo hili limetokea mara nyingi na miradi nyingine ambapo hatimaye tulipoteza ardhi kwa uhifadhi, uwindaji na kwa wawekezaji.”

# MAPENDEKEZO

Biashara ya hewa ukaa sio suluhisho la mabadiliko ya tabianchi. Upunguzaji wa hewa ukaa na Biashara yenyewe huku afrika haipaswi kuwa njia mbadala ya kupunguza utoaji wa hewa ukaa wa nchi za magharibi kule kwao.

**Ili kuhakikisha kwamba Biashara ya hewa ukaa haiathiri vibaya jamii za Wamasai tunapendekeza yafuatayo:**

1. **Serikali ya Tanzania inapaswa kusitisha mikataba yote ya hewa ukaa ya udongo na majadiliano kati ya jamii na wadau wa mradi wa hewa ukaa hadi mchakato sahihi wa ridhaa iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) utakapo zingatiwa. Kwa madhumuni hayo:**

   a. Biashara zote za hewa ukaa ya udongo katika nyanda za malisho za wafugaji zinapaswa kusitishwa angalau hadi 2030 ili kuruhusu jamii zetu kupata taarifa kamili na uelewa kuhusu hewa ukaa ya udongo na kuhakikisha kwamba hewa ukaa haihatarishi mustakabali wa wafugaji. Kwa vile uchaguzi mkuu utafanyika mwaka wa 2025, muktadha wa sasa unakabiliwa na siasa na rushwa.

   b. Mfumo wa kisheria wa Tanzania kuhusu miradi ya hewa ukaa ya udongo inayolinda haki za binadamu na ardhi za wafugaji unapaswa kutungwa.

   c. Katika ngazi ya kimataifa, kanuni zilizo wazi za soko la hewa ukaa la hiari zinahitaji kufafanuliwa, na zile za soko la lazima (soka la utii) la hewa ukaa zinahitaji kuboreshwa ili kuhakikisha kuwa haki za Watu wa Asili na jamii za wenyeji zinaheshimiwa.

2. **Ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) inapaswa kuzingatiwa katika hatua zote, kuanzia utambuzi wa mradi hadi uundwaji, utekelezaji na kufungwa. FPIC inapaswa kupatikana kabla ya kuingia katika kandarasi zozote za hewa ukaa. Kwa kusudi hilo:**

   a. Hakuna makubaliano juu ya miradi ya hewa ukaa inapaswa kuingiwa bila ushirikishwaji kamili wa wanajamii wote na kupata elimu huru, taarifa na ushauri wa kisheria;

   b. FPIC (Ridhaa kamili iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa) isiishie kwenye halmashauri ya kijiji na watu wenye ushawishi tu; mchakato halali wa FPIC unapaswa kuhusisha hatua tatu zifuatavyo: Kwanza; juhudi mahususi lazima zifanywe ili kuwashirikisha kikamilifu wanawake, vijana na makundi yaliyotengwa katika jamii; Pili; mkutano wa kijiji ambao hauna akidhi ya angalau 2/3 ya wakazi wa kijiji na usio na uwiano wa kijinsia hauwezi kuchukuliwa kuwa halali. Watu wazima wote kijijini lazima washirikishwe kikamilifu na kushauriwa; Tatu; mchakato wa FPIC ujumuishe jamii zote za Wamasai zinazoweza kuathiriwa na mkataba wa hewa ukaa, kama vile Wamasai wengine wanaoshiriki eneo moja la malisho, hata kama si wakazi wa kijiji hicho;

c. Taarifa zisizoegemea upande wowote, za uwazi na huru zinapaswa kutolewa, ili kuruhusu jamii zetu kutathmini manufaa na hasara ya miradi zinazopendekezwa. Hii ni pamoja na mafunzo sahihi, majadiliano na ushauri wa kisheria unaojitegemea na unaoaminika kwa wanajamii wote, huku msisitizo ukiwa kwa wanawake na vijana. Kwa kuongeza, mchakato wa FPIC haupaswi kufanywa na wadau wa mradi wa hewa ukaa.

d. Uwazi juu ya mikataba, mtiririko wa fedha, taratibu za malalamiko, na majukumu na wajibu wa wahusika na watu binafsi wanaohusika inapaswa kueleweka; Mikataba isiwe ya siri na iwe kwa Kiswahili na Kiingereza lakini ifafanuliwe kwa wanajamii katika lugha ya Maa;

e. Taratibu zinazojitegemea, zinazopatikana na zinazofaa kiutamaduni za ufuatiliaji, mrejesho, malalamiko, rufaa na usuluhishi zinapaswa kuafikiwa na pande zote mbili na jamii ikiwa ni pamoja na kupitia mikutano yake ya vijiji na isihusishe wadau wa kisiasa.

f. Wadau wa miradi wa hewa ukaa wanapaswa kuwa na sera ya umma na ya kina ya FPIC ambayo inaheshimu haki za binadamu na inaweza kufuatiliwa na jamii na mashirika ya kiraia.

g. Wadau wa miradi wa hewa ukaa wanapaswa kuweka wazi na kutoa mipango ya kina ya kugawana faida na kuweka ulinzi wa kimazingira na kijamii ili kuhakikisha miradi ya hewa ukaa haiathiri mfumo wa matumizi ya ardhi ya wafugaji, utamaduni wa jamii na desturi za jadi za matumizi ya ardhi. Wanapaswa kufichua na kuweka wazi habari zote muhimu kuhusu mnunuzi wa hewa ukaa ili kuhakikisha uwajibikaji.

3. **Carbon credit projects should neither interfere with nor undermine in any way pastoralism, access to natural resources such as water, grazing areas, firewood, access to sacred sites, traditional knowledge and land-use practices. For that purpose:**

a. Miradi ya Biashara ya hewa ukaa isiingilie uhamaji wa wafugaji kwa namna yoyote ile na inapaswa kuwezesha jamii zetu za Wamasai kudumisha udhibiti kamili wa ardhi yetu na kuwa wao ndio wanaofanya maamuzi kikamilifu juu ya wapi tutafuga na ni kwa wakati gani.

b. Miradi ya Biashara ya hewa ukaa inapaswa kuheshimu na kutoingilia mipango ya matumizi ya ardhi iliyopo. Wanapaswa kutafakari na kuheshimu kanuni zilizowekwa tayari za mpango shirikishi ya matumizi ya ardhi.

c. Miradi ya Biashara ya hewa ukaa inapaswa kuhakikisha kikamilifu na kulinda kimkataba usalama wa umiliki kisheria wa ardhi yetu; Biashara ya hewa ukaa haipaswi kuweka njia ya itakayopelekea kupokwa zaidi kwa ardhi ya Wamasai kuwa maeneo ya hifadhi, maeneo ya uwindaji na matumizi mengine yoyote isipokuwa ufugaji au chaguzi za maisha zilizoamuliwa na jamii za Masaai zenyewe.

d. Miradi ya Biashara ya hewa ukaa haipaswi kufunga jamii katika mikataba ya muda mrefu ambazo haziruhusu kusitishwa kwa urahisi na ukaguzi wa mara kwa mara na kuingilia kati mipango iliyopo au ya baadaye ya matumizi ya ardhi.

e. Jamii zinapaswa kuwa na uwezo wa kutengeneza tafiti zao za kimsingi ikiwa ni pamoja na kiasi cha hewa ukaa ya udongo kwenye ardhi yao; wana haki ya kupata taarifa kamili na za uwazi zilizokusanywa kwenye ardhi yao (itifaki ya msingi).



"Tunahofia kuwa kutokana na biashara ya hewa ya ukaa, kutakuwa na mipaka na marufuku kwa mpango wa ardhi ya malisho na kwa ujenzi wa nyumba. Mambo kama haya ya marufuku tumeshayaonja kwa maeneo ya mapito ya wanyama pori na katika maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori (WMAs).Kila wakati tunapoteza ardhi."

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1: HALI YA ARDHI NA HEWA UKAA KATIKA VIJIJI 11

***Jedwali la 1: vijiji vilivyotembelewa, umiliki wa ardhi na hali ya ushirikiano na wadau wa mradi wa hewa ukaa***

| Kijiji | Umiliki wa ardhi | Hatua iliyofikia kwenye mradi wa hewa ukaa |
|---|---|---|
| **Eluai** | Inayo CCRO ya pamoja, cheti cha ardhi ya kijiji na mpango wa matumizi bora ya ardhi (uliofanywa na UCRT (2021-2031). | • Imeingia mkataba kamili na Soil for the future (SftF).<br>• Kulikuwa na mikutano mikuu mitatu ya vijiji. Kwenye mikutano miwili walikubali kuingia mkataba, katika mkutano mkuu wa tatu waliamua kuvunja mkataba.<br>• Kishika uchumba (Milioni 51 TZS Takriban Dola za kimarekani 20,000/=) kwenye akaunti ya benki ya kijiji, akaunti ya benki ya kijiji imefungiwa kwa sababu ya mradi wa hewa ukaa.<br>• Uongozi wa Serikali ya kijiji uliangushwa kwenye uchaguzi uliopita kutokana na Biashara ya hewa ya ukaa.<br>• Utaratibu wa kusitisha mradi wa hewa ukaa ulianza baada ya maandamano ya wanakijiji, hawajafurahishwa na mkataba wa hewa ukaa ingawa bado haujakamilika kwa sababu ofisi ya DC/DED haifuatilii.<br>• Mchakato wa usuluhushi haujaanza na haujaeleweka namna ya kwenda mbele. |
| **Ngoswak** | Inayo CCRO ya pamoja, cheti cha ardhi ya kijiji, mpango wa matumizi bora ya ardhi (2019 2029). | • Imesaini mkataba na Soil for the Future.<br>• Imepokea pesa za uchumba (Milioni 40 TZS). |
| **Simonik** | Inayo CCRO ya pamoja, cheti cha ardhi ya kijiji, mpango wa matumizi bora ya ardhi (2019-2029). | • Imesaini mkataba na Soil for the Future.<br>• Imepokea pesa za uchumba (Milioni 52 TZS ). |
| **Lepruko** | Inayo CCRO ya pamoja, cheti cha ardhi ya kijiji na mpango wa matumizi bora ya ardhi (2019-2029). | • Haijaingia kwenye mkataba wa biashara ya hewa ukaa yoyote bali inapakana na vijiji 2 ambavyo vimefikiwa na wadau wa mradi (Mbaashi na Eng’arooji).<br>• Eneo lao la malisho linaingiliana na vijiji hivyo. |

| Kijiji | Umiliki wa ardhi | Hatua iliyofikia kwenye mradi wa hewa ukaa |
|---|---|---|
| **Engushai** | Haina CCRO ya pamoja, haina mpango wa matumizi bora ya ardhi na wala haina cheti cha ardhi ya kijiji. Engushai iliundwa upya baada ya Orkeju Kijiji cha Longishu kugawanywa. Kijiji cha Engushai bado hakijawekewa mipaka. | • Engushai ambayo ina (CCRO) moja na OrkejuLoongishu) imetia saini barua ya nia na Soil for the future kwa siku zijazo. Orkeju Loongishu imetia saini barua ya nia na TNC.<br>• Engushai haitaki kuendelea na makubaliano na soil For The Future na waliandika barua kwa UCRT/TNC kueleza nia yao ya kuingia nao mkataba katika mradi wa hewa ukaa ya udongo. |
| **Armanie** | Inayo CCRO ya pamoja, mpango wa matumizi bora ya ardhi na cheti cha ardhi ya kijiji ambacho si halali tena. Armanie iligawanywa na kuunda kijiji kingine kipya kinachojulikana kama kijiji cha Olopolosek.Kijiji cha Armanie na kijiji cha Olopolosek bado hazijapimwa na kuwekewa mipaka. | • Imesaini barua ya nia na Soil for the future ambayo muda wake umekwisha. Lakini haitaki kuendelea na makubaliano na soil for The Future na waliandika barua kwa UCRT/TNC kueleza nia yao ya kuingia nao mkataba katika mradi wa hewa ukaa ya udongo. |
| **Losirwa** | Inayo CCRO ya pamoja na mpango wa matumizi bora ya ardhi (2017-2027) na hati ya ardhi ya kijiji. | • Imesaini barua ya nia na TNC. |
| **Mswakini** | Inayo CCRO ya pamoja, mpango wa matumizi bora ya ardhi (2019-2029) na cheti cha ardhi ya kijiji. WMA haina CCRO. | • Inayo WMA kwenye ardhi ya kijiji.<br>• Inayo mgogoro wa mipaka na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.<br>• Mamlaka husika (Authorized Authority) imetia saini barua ya nia na TNC. |
| **Loondolwo** | Inayo CCRO ya pamoja, mpango wa matumizi bora ya ardhi (2015-2025 ) na hati ya ardhi ya kijiji. | • Imesaini mkataba na Soil for the Future.<br>• Imepokea pesa za uchumba (Milioni 70 TZS ) |
| **Magadini** | Inayo CCRO ya pamoja, mpango wa matumizi bora ya ardhi (2021-2031) na hati ya ardhi ya kijiji. | • Ilikuwa na majadiliano na Soil for the Future.<br>• Na sasa kipo katika mazungumzo na UCRT/TNC. |
| **Engaruka Juu** | Inayo CCRO ya pamoja, mpango wa matumizi bora ya ardhi (2019-2029) na cheti cha ardhi ya kijiji. | • Imesaini mkataba na Soil for the Future. |

# KIAMBATISHO CHA 2: UCHAMBUZI MUHIMU WA KISHERIA WA MAKUBALIANO YA HEWA UKAA:

Baadhi ya vifungu vyenye matatizo katika uuzaji wa SftF wa mikataba ya hewa ukaa ya udongo ni pamoja na:

1. **Muda wa mkataba:** Kifungu cha 4.1 kinatoa muda wa miaka 30 na 4.2 kinatoa chaguo la kuendeleza kwa miaka 10 ya ziada. Muda huu mrefu unaweza kukinzana na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ambayo inaweza kupitiwa kila baada ya miaka kumi. Itapunguza uamuzi wa kijiji kutumia ardhi hiyo kwa madhumuni mengine kwani kufanya hivyo ni sawa na kuvunja mkataba na matokeo yake ni dhahiri kwa mujibu wa kifungu cha 17.
2. **Kifungu cha FPIC:** Kifungu cha 7.1.3 kinahitaji ushahidi wa ridhaa iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) yaani kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kijiji. Hata hivyo, haihakikishi mchakato kamili na ufaao wa ridhaa iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC) (tazama mjadala wetu kuhusu ridhaa iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC).
3. **Vifungu vya kukomesha:** Kifungu cha 17.1 kinaruhusu kusimamishwa kazi na upande wowote baada ya kutoa notisi ya miezi 6. lakini, matokeo ya kukomesha ni ya upande mmoja. Kifungu cha 17. 2 kinatoa ahueni tu kwa mtoa pendekezo wa hewa ukaa na kuacha kijiji. Iwapo kijiji kitakatisha mkataba, mtoa pendekezo ataweza kutumia ardhi hiyo kwa miaka 3 (yaani kuendelea kuuza hewa ukaa kutoka katika ardhi hii) ili kufidia hasara/gharama zilizotumika. Zaidi ya hayo, hakuna rejea ya fidia itakayotolewa kwa kijiji endapo mhusika atakatisha mkataba. Kifungu cha 17.3 kinatoa unafuu mwingine kwa mtoa pendekezo kwa njia ya mthamini mwenye sifa ambaye ataletwa kufanya tathmini ya hasara na gharama zote alizotumia mtoa pendekezo, kulipwa na vijiji. Hii ni sehemu yenye matatizo sana ya mkataba kwa sababu itajumuisha gharama zote zilizotumika tangu mwanzo hadi wakati wa kusitishwa. Nani atamlipa mtoa pendekezo baada ya tathmini? Je, vijiji vina pesa za kulipa? Je, wakishindwa kumlipa mtoa hoja, itakuwa na athari gani kwenye usalama wa ardhi? Hatimaye, je, masharti yaliyo katika Vifungu 17.2 na 17.3 yanajumlisha? Kifungu cha 17.2 kinampa mtetezi haki ya kutumia ardhi hiyo kwa miaka 3 baada ya kusitishwa huku Kifungu cha 17.3 kinazungumzia fidia ya hasara iliyotokea na gharama baada ya tathmini. Je, masharti haya yanatumika kwa wakati mmoja? Je, mchakato utakuwa wa uwazi kiasi gani hasa katika suala la tathmini ya gharama?
4. **Wajibu wa afisa wa sheria wa wilaya:** Ushiriki wa wakili wa serikali kama shahidi[22] na kama wakili anayesimamia uingiaji wa makubaliano ni tatizo, kwa sababu ya mgongano wa kimaslahi (kwa vile wilaya inapokea sehemu fedha ya hewa ukaa iliyouzwa).
5. **Utaratibu wa utatuzi wa migogoro:** Mkuu wa wilaya amepewa mamlaka chini ya kifungu cha 19.2 cha kupatanisha wahusika ndani ya siku 30. Mkuu wa wilaya, kama mtumishi wa serikali (au mteule wa serikali) anafanya kazi kwa maslahi ya serikali. Kwa kuwa wilaya (pamoja na taasisi na wizara zingine za serikali) ni wanufaika wa moja kwa moja wa mradi wa hewa ukaa (kwa sasa 8% ya mapato yanapaswa kwenda wilayani), wilaya inaweza kutokuwa na nia ya kusitisha mkataba wa hewa ukaa.
6. **Kifungu cha Usiri:** Kuwepo kwa kifungu cha usiri hakuungi mkono mchakato wa uwazi na shirikishi wa ridhaa iliyo hiari, huru, iliyohabarishwa na kushirikishwa (FPIC).

*22 Kwa vitendo, mchakato wa kusaini mikataba ya kaboni unawezeshwa na Afisa Sheria wa Wilaya. Hakuna kijiji chenye wanasheria wao hivyo inategemea huduma za kisheria kutoka Halmashauri ya Wilaya. Kiuhalisia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini Tanzania imekuwa ikitumiwa na vyombo vya dola na watu binafsi kuchukua ardhi ya kijiji*

Baadhi ya vifungu vyenye matatizo katika mikataba ya ugavi wa faida ya SftF ni pamoja na:

1. **Matumizi ya ardhi:** Katika dibaji ya mkataba, aya C inakataza kwa uwazi na lugha isiyo na utata matumizi ya ardhi kwa matumizi mengine yoyote wakati kipindi chote cha mkataba.
2. **Wajibu wa halmashauri ya wilaya:** Mkataba unatambua katika Kifungu cha 3.1. halmashauri ya wilaya kuwa ni sehemu ya mkataba wakati ardhi ni mali ya kijiji. Kijiji ni chombo halali cha kisheria cha shirika chenye mamlaka kamili ya kufanya maamuzi bila kuingiliwa.
3. **Kutokuwa na uhakika:** Haijulikani ni lini kijiji kinaanza kupata mapato. Imeachiwa kampuni ya hewa ukaa kuamua wakati wa kuuza hewa ukaa na kushirikisha faida kwa kijiji. Ingawa kutokuwa na uhakika ni asili ya masoko ya hiari ya Biashara ya hewa ukaa, si haki kuhamishia mzigo wote wa mashaka na kutokuwa na uhakika kwa jamii.
4. **Utekelezaji wa mradi:** Vijiji vinatakiwa kutunza stakabadhi zote na ripoti za fedha na kupewa Kampuni ya hewa ukaa ikihitaji wakati wa utekelezaji wa mradi. Lakini kifungu kiko kimya juu ya majukumu ya Kampuni ya hewa ukaa. Tazama Kifungu 5.2.3 na 5.2.4. Kandarasi hiyo pia inaruhusu kampuni ya hewa ukaa kuingia na kukagua majengo na miradi mingine ambayo ilijengwa kupitia pesa iliyolipwa. Ndio kusema, kampuni ya hewa ukaa inapewa mamlaka makubwa sana ya kufuatilia matumizi ya fedha zilizolipwa huku ikiwa haijaweka mazingira ya uwajibikaji kwa upande wa kampuni. Tazama kifungu cha 5.3
5. **Kukoma kwa mkataba:** Kifungu cha 10.1 (a) kinaruhusu kijiji kusitisha mkataba endapo kampuni "itashindwa kulipa kijiji wakati utakapowadia". Nini maana yake wakati utakapowadia"? Zaidi ya hayo, kifungu hiki kinaruhusu kusitishwa kwa mkataba baada ya kutoa notisi ya miezi sita na hali hiyo haijatatuliwa ndani ya miezi mitatu (siku 90) na hivyo itafanya jumla ya miezi tisa kabla ya kusitisha mkataba. Huu ni wakati mwingi ambao unaelekea kufaidisha kampuni ya hewa ukaa na kunyonya kijiji. Aidha, Ibara ya 10.2 inazungumzia miaka mitatu ya matumizi ya ardhi baada ya kusitishwa. Vifungo hivi vinapaswa kupitiwa upya na kusawazisha masharti tatanishi kuwekwa bayana.
6. **Usuluhishi:** Kama ilivyojadiliwa hapo juu, Kifungu cha 13.2 kinaruhusu ofisi ya mkuu wa wilaya kupatanisha pande zote. Hili halifai kwa sababu ofisi iliyotajwa ni mteule wa mtendaji hivyo si mwakilishi wa wananchi.



“Tulishaweka saini ya makubaliano kwa mradi wa kaboni lakini sasa tunataka kuuvunja mkataba huu. Hatutaki kuwa na mgogoro na wanavijiji jirani zetu ambao hutumia ardhi yetu nyakati za kiangazi na ukame. Tumeshakuwa na makubaliano ya kushirikiana matumizi ya ardhi kwa miaka nyingi, na kwa ujio wa biashara ya hewa ya ukaa utaratibu huo hautakuwepo tena. hawataweza tena kuja kwetu.”

Baadhi ya vifungu vyenye matatizo katika Barua za Kusudio za TNC ni pamoja na:

1. **Asili ya hati:** Makubaliano yanaitwa Barua ya Kusudio au nia lakini inaonekana zaidi kuwa ni mkataba. Kifungu cha muda (Muda F) kina athari kubwa kwa kijiji. Kwa kusema kwamba Barua ya Kusudio itaendelea kutumika hadi pande zote mbili ziingie katika mkataba kamili, inafunga kijiji kwa muda usiojulikana bila muda kuwekwa wazi. Hii ina maana kwamba ikiwa mkataba wa mradi wa hewa ukaa utachukua miaka, au hata muongo mmoja kukamilika, kijiji kimefungwa kisheria na makubaliano haya na hakiwezi kutafuta fursa nyingine. Kipindi hiki cha kusubiri kwa muda usiojulikana kinaweka kijiji katika hasara kubwa, kwani kinawazuia kujadili mikataba bora na washirika wengine au kujihusisha katika miradi mingine yenye manufaa. Kutokuwepo kwa tarehe iliyo wazi ya kusitisha mkataba kunamaanisha kuwa jumii inasalia katika mkanganyiko wa kisheria, bila kufahamu ni lini makubaliano hayo yataisha.
2. **Mkanganyiko wa kisheria:** Moja ya Barua za nia tuliyochunguza ilitiwa saini Machi 2024 na ilipaswa kuanza Juni 2024. Kijiji bado hakijaingia mkataba kamili wakati muda imepita. Barua ya nia pia iko kimya juu ya matokeo na athari ya kutosainiwa kwa mkataba hadi sasa kwenye wajibu na athari kwa kijiji.
3. **Muda wa Mkataba:** Muda wa mkataba kamili unaotarajiwa ni miaka 20 na hailezi kama itaongezwa muda wake wakati kwenye Barua iliyowasilishwa Verra inaonyesha kuwa mkataba unastahili kuwa miaka 40.
4. **Wakati wa kusitishwa:** Pande zote mbili zinaweza kusitisha makubaliano ya kuingia mkataba wa hewa ukaa kwa kutoa notisi ya siku 60. Barua ya Kusudio iko kimya juu ya athari za kusitisha.
5. **Kuhusu mchakato wakati wa mgogogo:** Barua ya Kusudio inaeleza kuwa mgogoro inaanza kusuluhishwa kwa njia ya mazungumzo. Iwapo mazungumzo yatashindikana basi suala hilo litapelekwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya. Ikishindikana suala hilo litaenda kwa Mkuu wa Wilaya na uamuzi wake utakuwa wa mwisho. Vyombo viwili vya mwisho vya rufaa ni wafanyikazi wa serikali na uzoefu unaonyesha kuwa kila wakati wanaegemea upande wa wawekezaji. Hakuna mchakato wa kimahakama.
6. **Jukumu la afisa wa sheria wa wilaya:** Kuhusika kwa mwanasheria wa serikali kama shahidi na kama wakili anayesimamia uingiaji wa makubaliano ni dosari, kama inavyoonekana hapo juu katika suala la SftF.

## MUUNGANO NA MSHIKAMANO WA KIMATAIFA WA MAASAI MSHIKAMANO (MISA)

**Muungano na Mshikamano wa Kimataifa wa Maasai (MISA) ni muungano wa kimataifa unaosimama kwa mshikamano na Wamasai wa Kaskazini mwa Tanzania. Tunaleta pamoja mashirika ya kimataifa ya kidini, mashirika ya haki za binadamu, mashirika ya kimataifa ya misaada na maendeleo, pamoja na mashirika ya ndani ya Tanzania, wanaharakati binafsi, watafiti na wanasheria wanaowawakilisha Wamasai katika kesi kadhaa za ardhi.**

Muungano wetu unajumuisha, miongoni mwa mengine, the Africa Europe Faith Justice Network (AEFJN), Agrecol Association for AgriCulture & Ecology, Coalition of European Lobbies for Eastern African Pastoralism (CELEP), Center for Agroecology, Water and Resilience (CAWR) at Coventry University (UK), CIDSE - International family of Catholic social justice organisations (International), Indigenous Movement for Peace Advancement and Conflict Transformation (IMPACT), FIAN International, FINAL GOVERNANCE, KOO (Koordinierungsstelle der Österreichischen Bischofskonferenz (Coordinating Office of the Austrian Bishops' Conference), Gesellschaft für bedrohte Völker (Society for Threatened Peoples), Misereor, PALISEP, PINGO's Forum (Pastoralists Indigenous Non-Governmental Organisations), PWC (Pastoral Women's Council), TEST (Traditional Ecosystems Survival Tanzania), UCRT (Ujamaa Community Resource Team) and Welthaus Graz. Lengo letu kuu ni kukomesha ukiukwaji wa haki za binadamu unaowakabili Wamasai wa kaskazini mwa Tanzania.

“Tunahitaji kuelimishwa zaidi na kuwa na uelewa mpana.- na kiuhalisia tunahitaji kuwa na uelewa wa kina kabla hatujaingia katika makubaliano ya aina yeyote.”





**Kunukuu ripoti hii:**

**Biashara ya Hewa ya Ukaa ya Udongo Katika Ardhi ya Wamasai: Wimbi Jingine la Kutwaliwa kwa Ardhi?**
Ripoti ya Utafiti ya Muungano wa Kimataifa wa Mshikamano na Maasai Wamaasai (MISA). Machi 2025

**Maasai International Solidarity Alliance (MISA)**

Kwa habari zaidi: maasaiinternationalsolidaritya@gmail.com